

WANYAMA TUNA UHURU

Pulikeni ndugu naja, kunena yalo yakini,
Ni maonevu ya waja, wanotutesa njiani,
Twapigwa hata mapaja, usoni na mgongoni,
Na sisi wanyama piya, uhuru twauliliya.

Si punda sio ngedere, sisi sote twateseka,
Mizigo tuiburure, kwa pulau tunavuta,
Twanyimwa hata na pure, piya tonge tulosaka,
Na sisi wanyama piya, uhuru twauliliya.

Twahitaji na maziwa, afiya tuimarishe,
Tupate maji kunywiwa, mengine wayachemshe,
Tuoge bila makiwa, miili tuburudishe,
Na sisi wanyama piya, uhuru twauliliya.

Twafaa kupumzika, baada ya nyingi gange,
Malazi yakulainika, wala siyo makonge,
Tuwe kama malaika, washibao kwa matonge,
Na sisi wanyama piya, uhuru twauliliya.

Twataka nafasi piya, ya kucheza kila mara,
Tuimbe hata hodiya, tuwaliwaze na swara,
Wasije tena kuliya, kwa kuvishwa matambara,
Na sisi wanyama piya, uhuru twauliliya.